8 -12 Kanuni ya Maadili ya Wanafunzi naMwongozo wa Viwango wa Ukosaji

Vitendo vya kiwango cha 1 si vya nguvu sana. Vitendo vya kiwango cha 1 si lazima vionyeshe tishio katika afya, usalama au mali za wengine. Hatua chanya za darasani na shule nzima na usaidizi zinatumiwa kushughulikia vitendo vya Kiwango cha 1. Wanafunzi hawapelekwi kwa msimamizi kwa vitendo vya Kiwango cha 1 isipokuwa wataendelea baada ya hatua kuchukuliwa na kupewa usaidizi. Katika mazingira kama hayo, kupelekwa kunamaanisha kusaidia kubainisha njia zinazofaa zaidi zilizopo kwa ajili ya mwanafunzi.

101.A. **Kuchelewa Kufika Shuleni:** Kuwasili baada ya muda wa kuanza bila ruhusa iliyoandikwa, halali.

101.B. **Kuchelewa Kufika Darasani:** Kuwasili baada ya muda wa darasa kuanza bila ruhusa iliyoandikwa, halali.

102. **Utoro au Kutohudhuria kwenye Darasa:** Kutohuduria darasani au shuleni bila ruhusa.

103. **Mali Binafsi Zisizofaa:** Kumiliki na/au kutumia vitu ambavyo vinasababisha usumbufu katika kujifunza, kuharibu mali ya mtu, au vinginevyo kuvuruga mchakato wa kujifunza. Vitu visivyofaa ambavyo ni mali binafsi vinaweza kujumuisha lakini si tu, vifaa vya kielektroniki, vitu vya kuchezea, karata, kofia, mavazi, chakula kisichoruhusiwa, dawa ambayo haijasajiliwa na muuguzi wa shule chini ya Sera ya 229 – Matumizi ya Dawa, na Sera 229.1 – Kumiliki/Kutumia Dawa za Dharura.

104. **Kusumbua, Kuchokoza au Mchezo wa kusukumana:** Mawasiliano ya ana kwa ana na mwanafunzi mwingine ambayo yanafanywa kwa makusudi yasiyo ya kielimu na ama yanaingiliana na elimu au usalama wa mazingira ya shule.

105. **Lugha au Ishara Zisizofaa:** Maoni ya maandishi au ya kutamka au ishara ambazo zinatweza, kudharau au kumdhalilisha mtu au kundi la watu kupitia matumizi ya maneno au vitendo, ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha mbaya au ya matusi.

106. **Kutozingatia Sheria za Basi Zilizobandikwa**: Kukiuka sheria za basi au shule zilizobandikwa au kuandikwa; mifano: kutokaa kwenye kiti chako, kutofuata maelekezo ya mfanyakazi au kupanda au kushuka kwenye kituo cha basi kisicho sahihi.

107. **Kutozingatia Sheria za Shule Zilizobandikwa**: Ukiukaji wa sheria au kanunu mahususi za shule au darasani zilizobandikwa au kuandikwa. Mifano inajumuisha lakini si tu: kutafuta bigiji kwa kurudiarudia, kuzungumza darasani kwa kurudiarudia, kukimbia, kurusha vitu na kukiuka sheria za mavazi.

111. **Kumiliki Vifaa vya Kielektroniki au Mawasiliano.** Wanafunzi wanaweza kuwa na vifaa vya kielektroniki kulingana tu na ilivyoruhusiwa na sera ya Bodi na sheria za shule. Kamati za Nidhamu za shule zinaweza kuweka makatazo hayo kwa namna inayolingana na Sera ya Bodi 216 – Vifaa vya Kielektroniki. Maelezo mahususi kuhusiana makatazo ya kifaa cha kielektroniki yatatolewa mapema kwa wanafunzi na wazazi/walezi kabla ya kutekeleza katazo lolote.

Makatazo ya vifaa vya kielektroniki hayatatumika wakati ambapo mwanafunzi (1) ni mshiriki wa kujitolea wa kampuni ya zima moto, gari la wagonjwa, au kikosi cha wokozi; au (2) ana uhitaji wa kifaa hicho kwa sababu ya hali ya kiafya mwanafamilia wa karibu.

Wanafunzi wanaokiuka makatazo ya vifaa vya kielektroniki wanaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kupokonya kifaa hicho.

112. **Kuvuruga Ratiba za Darasani**: Tabia ya maneno ya kimwili ambayo imeamuliwa na mwalimu wa

darasa kuwa inavuruga mafunzo. Mifano inajumuisha lakini si tu: kupiga kelele kwa kurudiarudia darasani au kwa kupokezana, kuwa na sauti ya juu kuliko wangine, kukimbiakimbia, kurusha vitu, kushindwa kufuata sheria za darasani.

114. Kutumia Vibaya Kompyuta/Mitandao ya Kompyuta/Kifaa cha Kielektroniki: Mwanafunzi hatajihusisha na kitendo chochote kinchokiuka Sera ya Wilaya ya Matumizi ya Mtandao na Usalama, miongozo yoyote ya matumizi ya kompyuta ya shule au miongozo ya matumizi ya kifaa cha mkononi, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu vitendo vifuatavyo ambavyo si lazima viweke hatari kwenye afya, usalama au mali za wengine:

A. Kutumia kompyuta, mitandao ya kompyuta au vifaaa vya kieletroniki katika nyakati ambapo vitendo hivyo haviruhusiwi

B. Kupakia au kutumia kwa kukusudia michezo, programu, mafaili au maudhui mengine ya kielektroniki yasiyoidhinishwa, kwenye vifaa vya Wilaya

C. Kutumia utambulisho wa mtumiaji mwingine, kutojibainisha jina na majina bandia, ndani ya mifumo ya Wilaya

D. Kutengeneza viungo vya kwenye mitandao mingine ambavyo maudhui au makusudi yake yanakiuka Sera ya Wilaya ya Matumizi ya Matumizi na Usalama

E. Mawasiliano ya kuudhi ambayo hayaweki hatari kwenye usalama

F. Ustaarabu mzuri katika matumizi ya mtandao utafundishwa na kutekelezwa kabla ya kuendelea na kutoa adhabu kwa ajili ya ukiukaji wa matumizi sahihi ya kompyuta.

Kiwango cha 1 - Mifano ya Uingiliaji kati wa Mwongozo (Mbadala wa Adhabu za Kipekee)
Orodha iliyo hapa chini imetolewa kama menyu ya machaguo yanayoweza kuwepo na haikusudiwi kutumika kwa mfuatano. Utekelezaji wa uingiliaji kati utakuwa mahususi, badala ya mbinu ya kipimo kimoja kinawatushea wote.

- Kutumia Mbinu za Urejeshaji (yaani, kauli zenye ufanisi, maswali ya kurejesha, vikundi mikutano ya baila maandalizi, n.k.)
- Rejea kwenye Mfumo wa Michezo wenye Ngazi Nyingi (MTSS) ili kupata sababu ya tabia hiyo
- Kutumia PBIS kufundisha tena darasani na matarajio ya shule nzima
- Kuelekeza kwenye mipango ya utatuzi wa migogoro ya shuleni (k.m mapatano ya kundi rika)
- Mkutano wa wanafunzi na walimu
- Mkutano wa wazazi au waliezi/walimu
- Kufunisha tena/kuunda matarajio
- Mkutano wa mwanafunzi/msimamizi
- Mkutano wa uingiliaji kati unaofanywa na mfanyakazi wa ushauri
- Kazi ya kutafakari ya maandishi
- Endeleza, hakiki, au pitia nyenzo binafsi za kupangaza mwanafunzi (k.m Mpango wa Usaidizi wa Tabia)
- Mabadiliko kwenye ratiba au darasa (kwa kumwarifu mzazi/ mlezi)
- Ushauri nasaha kwa mtu binafsi/kikundi
- Kuelekeza kwenye Mpango wa Usaidizi kwa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuiaji (k.m, mafunzo ya ujuzi wa mihamko ya uhusiano wa kijamiikama vile kudhibiti hasira, kuondoa matumizi ya nguvu, ujuzi wa kupangilia mambo) na/au uingiliaji kati (k.m ushauri nasaha wa mazoea ya kiafya)
- Mkutano/mpango wa kuboresha mahudhurio shuleni

- Mpango wa tabia ya mwanafunzi
- Kuelekezwa kwenye mpango ushauri mafunzo
- Kuelekezwa kwenye Shirika la Kijamii Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)
- Huduma ya jamii (kwa idhini ya mzazi/mlezi)
- Mbadala mwingine unaofaa wa hatua za kinidhamu za kipekee (hatua za kinidhamu za kipekee hujumuisha kukamwatwa, kufukuzwa kwa muda ndani ya shule, kufukuzwa kwa muda nje ya shule)

Vitendo vya Kiwango cha 2 ni vya uzito mkubwa na vinaweza kuwa na tishio kwenye afya, usalama au mali ya mtu yeyote. Msimamizi anaarifiwa pale ambapo kitendo cha Kiwango cha 2 kinatokea. Wanafunzi walio katika gredi ya 6-12 wanaweza kufukuzwa shule kwa ajili ya vitendo vya Kiwango cha 2. **Vitendo vyenye alama ya nyota vinaanzisha arifa ya lazima kwenye polisi ya shule kwa mujibu wa Kifungu cha Kanuni ya Shule 1303-A(b) na 22 Pa. Kifungu cha Kanuni 10.22.**

202. Uharibifu au Uporaji wa Mali ya Shule (Vurugu*): Kusababisha au kujaribu kusababisha uharibifu kwenye mali ya shule.

203. Uharibifu au Uporaji wa Mali Binafsi (Vurugu*): Kusababisha au kujaribu kusababisha uharibifu mkubwa kwenye mali binafsi

209. Mwanafunzi Kuwepo Shuleni Bila Kuidhinishwa wakati wa Saa za Shule (*Si vurugu*):

209.A. Kwenye Viwanja vya Shule: Mwanafunzi hapaswi kuwa kwenye sehemu yoyote ya viwanja vya shule, ambapo uwepo wake haujaidhinishwa, wala kubaki baada ya ama kuamuriwa au kuombwa aondoke na mfanyakazi yeyote wa shule.

209.B. Kwenye Jengo Binafsi au la Umma: Mwanafunzi hataruhusiwa kuwepo kwenye sehemu yoyote ya jengo binafsi au la umma wakati wa saa fulani za shule. Wakati wa saa ya shule wanafunzi wanapaswa kuwa shuleni isipouwa kama wameruhusiwa kutokuwepo shuleni.

210. Kuvuta sigara, Muvuke na Matumizi ya Tumbaku (*Si vurugu*): Kuvuta sigara, kumiliki au kutumia tumbaku au kifaa chocgote cha kielektroniki cha kuvuta sigara katika majengo ya shule, mabasi ya shule, au kwenye majengo yoyote yanayomilikiwa na, kupangishwa na au chini ya udhibiti wa shule.

212. Kutokuwa mwaminifu kitaaluma (*Si ya vurugu*)**:** Kutokuwa mwaminifu kitaaluma kutajumuisha, lakini si tu, aina zote za udanganyifu, kuiba mawazo ya wengine, kuiba fomu za mitihani, kuwakilisha kazi ya mtu mwingine kama yake, na matumizi yasiyoidhinishwa ya vifaa saidizi, wakati wa mitihani, miradi na kazi.

213. Unyanyasaji (*Vurugu*): Aina ya unyanyasaji kwa msingi wa mbari, rangi, umri, kabila, dini, jinsi, jinsia (ikiwa ni pamoja na ubainishaji na utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kingono, asili, asili ya kitaifa, hali ya ndoa, ujauzito au ulemavu ikiwa ni pamoja na vitendo visisvyotakiwa, au vitendo vingine ambavyo vinaweza kuwa na madhara au vya kudhalilisha au kuingilia shule ya mtu au utendaji unaohusiana na shule pale ambapo kitendo hicho ni kibaya, kinadumu au kinapotosha na mtu wa kawaida katika sehemu ya malalamikaji anaweza kuona kwamba inaweka mazingira ya kielimu ya kuogopesha, kutisha au kunyanyasa..

Vitendo mahususi vya unyanyasaji vimefafanuliwa zaidi kama ifuatavyo:

***213.A. Unyanyasaji wa Kingono:** Kitendo cha kingono ambacho hakijakubaliwa na kinachukuliwa na mtu wa kawaida kuwa ni kibaya, kilichopotoka na cha uhalifu ambacho kinamnyima mtu husika ufikiaji sawa wa mpango wa Wilaya. Unyanyasaji wa kingono kwa

madhumuni ya kupewa upendeleo, kumhitaji mtu atoe ndono bila ridhaa yake kwa lengo la kupewa msaada, manufaa au huduma pia unashughulikiwa na sera ya Wilaya. Ukatili wa kingono, ukatili kwenye mahusiano, ukatili wa nyumbani na kumfuatilia mtu, kama ilivyofafanuliwa kwenye sera ya Wilaya pia ni aina ya unyanyasaji wa kingono.

213.B. Unyanyasaji wa Kimbari/Kabila Ubaguzi kwa msingi wa mbari, rangi au asili ya utaifa, ikiwa ni pamoja na ubaguzi kwa msingi wa mbari halisi ya mtu au inayodhaniwa, rangi, asili ya kitaifa, kabila au ukoo. Hii inajumisha ubaguzi kwa msingi wa nchi, dunia,au eneo, ambapo mtu au mababu zake wanatoka huko; mtu kutozungumza Kiingereza au hali ya Mjifunzaji wa Kiingereza; au asili halisi ya mtu au inayodhaniwa au sifa za kikabila, ikiwa ni pamoja na ushiriki katika dini ambayo inaweza kudhaniwa kuwa inaonyesha tabia hizo (kama vile, Wahindu, Wayahudi< Waislamu na Wasikh).

213.C. Unyanyasaji wa Kijinsia: unaweza kujumuisha vitendo maneno, visivyo vya maneno au vya kimwili vinavyoogopesha au vinavyojenga chuki kwa sababu ya mitazamo ya kijinsia. Kwa hivyo, unyanyasaji wa mwanafunzi kushindwa kufuata dhana za kibaguzi za uanaume na uanamke unajumuisha ubaguzi wa kijinsia. Unyanyasaji wa kijinsia unaweza kutokwa kwa kukiuka sera ya Wiliaya na/au Sura ya IX wakati kitendo hicho kinamnyima au kinazuia uwezo wa mwanafunzi kupokea msaada wa kieleimu, manufaa, huduma au kutendewa.

213.D. Unyanyasaji kutokana na Ulemavu Tabia za kuogopesha au unyanyasaji kwa mwanafunzi kwa msingi wa ulemavu ambao unatengeneza mazingira ya uadui kwa kuingiliana na au kumnyima mwanafunzi kushiriki au kupokea manufaa, huduma au fursa katika mpango wa taasisi. Matendo ya unyanyasaji yanaweza kujumuisha vitendo vya kutamka na matusi, vilevile tabia isiyo ya maneno kama vile kauli za grafiki na za maandishi au matendo ambayo yanatishia kimwili, yenye madhara, au yanadhalilisha.

213.E. Aina nyingine ya Unyanyasaji: Kitendo chochote kinachokiuka Katazo la Wiliaya la Sera ya Uchokozi/Unyanyasaji ambayo haikidhi fasili ya unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kimbari/kikabila, unyanyasaji wa kijinsia au unyanyasaji kutokana na ulemavu.

214. Kutumia Vibaya Kompyuta/Mitandao ya Kompyuta/Kifaa cha Kielektroniki (*Isiyo ya vurugu*)::
Mwanafunzi hatajihusisha kwa kukusudia na kitendo chochote kinchokiuka Sera ya Wilaya ya Matumizi ya Mtandao na Usalama, miongozo yoyote ya matumizi ya kompyuta ya shule au miongozo ya matumizi ya kifaa cha mkononi, au makubaliano yaliyosainiwa na wazazi wa mtoto kuhusu kuhusu matumizi ya nyenzo za teknolojia, ikiwa ni pamoja na lakini si tu yafuatayo::

A. Kutuma, kuchapisha, kufikisha au kumiliki ujumbe wa kielektorniki ambao ni wa kunyanyasa, wa uchi, wenye mweleko wa kingono, unaotisha, unaonyanyasa, unaoharibu sifa ya mwingine, au haramu, ikiwa ni pamoja na video za matendo yasiyofaa ya wanafunzi, uchokozi wa mtandaoni na ‘kutumiana ujumbe wa kingono,’ ama katika eneo la shule au nje ya eneo la shule ikiwa kitendo hicho kinasababisha vurugu kubwa katika mazingira ya kielimu kinakiuka haki za mwanafunzi mwingine shuleni.
B. Kujaribu kubadilisha, kuharibu au kuzima nyenzo za teknolojia ya Wilaya ikiwa ni pamoja na lakini si tu, kompyuta na nyenzo husika, data ya Wilaya, data ya wengine, au mitandao mingine inayohusiana na mfumo wa Wilaya, ikiwa ni pamoja na jengo la shule ikiwa kitendo hicho kinasababisha vurugu kubwa katika mazingira ya kielimu.

C. Kutumia intaneti au mawasiliano mengine ya kielektroniki kuwatishia au kuwanyanyasa wanafunzi wa Wilaya, wafanyakazi, wanabodi au wafanyakazi wa kujitolea, ikiwa ni pamoja na majengo yaliyo nje ya shule ikiwa yanasababisha vurugu kubwa kwenye mazingira ya kielimu au kukiuka haki za mwanafunzi mwingine shuleni.
D. Kutumia intaneti au mawasiliano mengine ya kielektroniki kujihusiaha au kuhamasiaha tabia haramu, au kutishia usalama wa shule, ikiwa ni pamoja na majengo yaliyo nje ya shule ikiwa kitendo hicho kinasababisha vurugu kubwa kwenye mazingira ya kielimu au kukiuka haki za mwanafunzi mwingine shuleni.
E. Kujaribu kufikia au kuharibu manenosiri au taarifa nyinginezo zinazohusiana na ulinzi wa Wilaya, wanafunzi au wafanyakazi, au maudhui yanayopakiwa au kutengeneza virusi vya kompyuta, ikiwa ni pamoja na katika jengo lililo nje ya shule ikiwa kitendo hicho kinasababisha vurugu kubwa katika mazingira ya kielimu.

Ustaarabu mzuri katika matumizi ya mtandao utafundishwa na kutekelezwa kabla ya kuendelea na kutoa adhabu kwa ajili ya ukiukaji wa matumizi sahihi ya kompyuta.

216. Ugomvi (*Vurugu*) : Kutumia vurugu za kimwili baina ya wanafunzi wawili, ambapo haiko wazi baada ya uchunguzi kufanywa ni mwanafunzi yupi aliyekuwa mchokozi au mwanzilishi wa ugomvi.

217. A. Uchokozi (*Vurugu*) : Uchokozi humaanisha kitendo cha kukusudia kupitia elektroniki, maandishi, maneno au kitendo halisi au mfululizo wa vitendo vinavyoelekezwa kwa mwanafunzi au wanafunzi wangine, ambacho kinatokea katika mazingira ya shule, ambacho ni kibaya sana, cha kuendelea au kupotosha chenye kusudi au nia ya:

1. Kuunda mazingira ya kuogopesha au ya chuki ambayo hatimaye yanaingiliana na elimu ya mwanafunzi au
2. Kumdhuru mwanafunzi, kimwili, kihisia au kiakili; au
3. Kumweka mwanafunzi katika hofu dhahiri ya madhara ya kimwili au kihisia; au
4. Kumweka mwanafunzi katika hofu dhahiri ya kuharibu au kupoteza mali binafsi ya mtu

217.B. Uchokozi wa mtandaoni (*Vurugu*) : Uchokozi hujumuisha uchokozi wa mtandaoni na/au uchokozi kupitia vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, mitandao ya kijamii, barua pepe, ujumbe wa papo hapo, ujumbe wa maandishi ujumbe wa Twitter (kwenye Twitter), blogu, kushiriki picha na video, vyumba vya kuchati, dshibodi au tovuti. Uchokozi unaweza kujumuisha vitendo ambavyo ninatokea nje ya shule ikiwa vigezo kadhaa vinakidhiwa.

Katazo kamili la Sera ya Uchokozi/Unyanyasaji, malalamiko na taratibu za uchunguzi unachaposhwa kwenye tovuti ya Wilaya kupitia www.pps.k12.pa.us/Page/481, na katika kila jengo na darasa.

218. Udhalilishaji (*Vurugu*) : Udhalilishaji unatokea pale ambapo mtu kwa kukusudia, kwa kujua au bila kujali, kwa kusudi la kuanzisha, kuingia au kumshirikisha mwanafunzi kwenye kikundi kwa kusudi la kuendelea au kuimarisha uanachama au hali katika kikundi, anasababisha au kumlazimisha mwanafunzi afanye yoyote kati ya haya yafuatayo:

1. Kukiuka sheria ya shirikisho au jimbo.
2. Kula chakula chochote, kimiminika, kimiminika cha pombe, dawa za kulevya au dutu nyingine yoyote ambayo inamweka mwanafunzi kwenye hatari ya madhara ya kihisia au kimwili.
3. Kustahimili ukatili wa asili ya kiakili, ikiwa ni pamoja na shughuli inayoathiri kwa kiasi kikubwa afya ya akili au utu wa mtu, kukosa usungizi, kujiondoa katika mikusanyiko ya kijamii au kitendo

ambacho kinaweza kusababisha fadhaa kubwa.

4. Kustahimili ukatili wenye asili ya kingono.
5. Kustahimili shughuli nyingine yoyote ambayo inaunda uwezekano wa madhara ya kimwili kwa mwanafunzi.

Shughuli hizo hapo juu zinachukuliwa kuwa ni udhalilishaji bila kujali iwapo idhini ya mwanafunzi ilitolewa au ilipatikana.

219. A. Maneno Machafu na Uhuni (Mwanafunzi) (*Isiyo ya vurugu*):: Matusi, kulaani kufanya ishara za kihuni, au kutumia lugha ya kuudhi kwa mwanafunzi mwingine.

219.B. Maneno Machafu na Uhuni (Mfanyakazi) (*Isiyo ya vurugu)*):: Matusi, kulaani kufanya ishara za kihuni, au kutumia lugha ya kuudhi kwa mfanyakazi mwingine.

220. A. Mapigano ya kimwili (Mwanafunzi) (*Vurugu*):: Mwanafunzi kufanyia mwanafunzi mwingine vurugu ambapo hakuna jeraha kubwa kama iliyoamuliwa na msimamizi wa shule, lakini kuna mchokozi aliye dhahiri au mwanzilishi wa ugomvi wa kimwili na wamekabana.

220.B. **Mapigano ya kimwili (Mfanyakazi) (***Vurugu*):: Mwanafunzi kufanyia mfanyakazi mwingine vurugu ambapo hakuna jeraha kubwa kama iliyoamuliwa na msimamizi wa shule, lakini kuna mchokozi aliye dhahiri au mwanzilishi wa ugomvi wa kimwili na wamekabana.

221. Vitisho vya Kigaidi (*Vurugu*): Kitisho kinachoonyeshwa moja kwa moja au isivyo moja kwa moja ili kufanya uhalifu wowote kwa kusudi la kuatia hofu wengine, kusababisha watu kuondolewa kwenye jengo, sehemu ya mkusanyiko au nyenzo ya usafiri wa umma, au vinginevyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa umma, au kusababisha hofu kubwa au usumbufu mkubwa kwa umma kwa kutokujali hatari ya kusababisha hofu au usumbufu huo mkubwa

222. Tabia za Kingono Zisizofaa (*Si ya vurugu*):: Kufunua au kushika sehemu za siri za mtu, matiti au matako au sehemu za kingono za mtu mwingine. Inaweza pia kujumuisha kujihusisha katika ngono, ngono ya kinywa au matendo ya kingono kwenye viwanja vya shule.

223. Kuchochea Usumbufu au Vurumai (Vurugu*): Kusababisha usumbufu mkubwa au ugomvi miongoni mwa kikundi cha watu, ikisababisha uingiliaji kati wa wafanyakazi kadhaa wa shule ili kutuliza usumbufu huo.

225. Vitisho/Kuogopesha (*Si vurugu*): : Kitisho cha kufanya fujo. Vitisho katika kiwango hiki cha uvunjaji sheria vinakuwa na hatari ya chini kwa mwathiriwa au usalama wa umma. Kitisho hiki hakiwi dhahiri na si cha moja kwa moja, taarifa zilizomo ndani ya kitisho si thabiti, hazina mashiko au hazina maelezo ya kina, kistisho hicho hakina uhalisia na maudhui ya kitisho yanaonyesha kwamba mtu huyo haelekei kukitekeleza. Vitisho vinaweza kufanywa kwa maneno, kwa maandishi au kwa ishara.

226.A. Wizi, Udokozi, au Ujambazi kwenye Majengo ya Shule (Vurugu*): Mwanafunzi hapaswi kujihusisha au kujaribu kujishusisha na wizi, udokozi au ujambazi kwenye majengo ya shule.

226.B. Wizi, Udokozi, *au* Ujambazi kwenye Majengo Binafsi (Vurugu*): Mwanafunzi haruhusiwi kuiba au kujaribu kumwimbia mwanafunzi mwingine au kufanya uvamizi kwenye jengo binafsi.

Kiwango cha 2 - Mifano ya Mwongozo wa Uingiliaji Kati
Orodha iliyo hapa chini imetolewa kama menyu ya machaguo yanayoweza kuwepo na haikusudiwi kutumika kwa mfuatano. Utekelezaji wa uingiliaji kati utakuwa mahususi, badala ya mbinu ya kipimo kimoja kinawatoshea wote.

- Kutumia Mbinu za Urejeshaji (yaani, kauli zenye ufanisi, maswali ya kurejesha, vikundi mikutano isiyo rasmi maandalizi, mikutano rasmi ya urejeshaji, n.k.)
- Kuelekeza kwenye michakato ya Mifumo ya Usaidizi ya Ngazi Nyingi (MTSS)
- Kuelekeza kwenye mipango ya utatuzi wa migogoro ya shuleni (k.m mapatano ya kundi rika, mikutano ya urejeshaji)•
- Mkutano wa wanafunzi na walimu
- Mkutano wa wazazi au waliezi/walimu
- Kufunisha tena/kuunda matarajio
- Mkutano wa mwanafunzi/msimamizi
- Mkutano wa uingiliaji kati unaofanywa na mfanyakazi wa ushauri
- Kazi ya kutafakari ya maandishi
- Endeleza, hakiki, au pitia nyenzo binafsi za kupangaza mwanafunzi (k.m Mpango wa Usaidizi wa Tabia)
- Mabadiliko kwenye ratiba au darasa (kwa kumwarifu mzazi/ mlezi)
- Ushauri nasaha kwa mtu binafsi/kikundi
- Kuelekeza kwenye Mpango wa Usaidizi kwa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuiaji (k.m, mafunzo ya ujuzi wa mihemko ya uhusiano wa kijamii kama vile kudhibiti hasira, kuondoa matumizi ya nguvu, ujuzi wa kupangilia mambo) na/au uingiliaji kati (k.m ushauri nasaha wa mazoea ya kiafya)
- Mpango wa tabia ya mwanafunzi
- Kuelekezwa kwenye mpango ushauri mafunzo
- Kuelekezwa kwenye Shirika la Kijamii Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)• Huduma ya jamii (kwa
- idhini ya mzazi)

- Mbadala mwingine unaofaa wa hatua za kinidhamu za kipekee (hatua za kinidhamu za kipekee hujumuisha kukamwatwa, kufukuzwa kwa muda ndani ya shule, kufukuzwa kwa muda nje ya shule)

Mifano ya Hatua za Kinadhamu Zinazopendekezwa Baada ya au Pamoja na Miongozo ya Uingiliaji Kati Inayotumika (Kiwango cha 2)

- Uzuiliwaji kama adhabu: Kazi kwenye mahali maalumu pa shule nje ya saa za masomo (k.m, kabla ya masomo, baada ya masomo, au katika siku isiyo ya masomo)
- Kufukuzwa shuleni kwa muda: Kusitishwa masomo na kazi kwenye sehemu maalumu ya kujifunzia. Kazi hii inaweza kupewa jina tofuati na “Kufukuzwa shuleni kwa muda” kwa kila mfumo wa PBIS wa shule Kufukuzwa kwa muda shuleni kunaweza kufanyika kulingana tu na utaratibu wa kiuongozi unaotolewa na Mrakibu na Mrakibu Msaidizi kwa ajili ya Huduma za Usaidizi kwa Mwanafunzi.
- Njia mbadala nyingine za kufukuzwa kwa muda nje ya shule
- Kuzuiliwa safari za uwandani, mikusanyiko, au manufaa mengine maalumu
- Kufukuzwa kwenye shughuli za ziada
- Kusitishwa kupata manufaa ya usafiri
- Kusitishiwa kushiriki katika matukio maalumu aupromosheni
- Kufukuzwa shuleni kwa muda kwa kipindi kifupi (siku 1–3)

Mwanafunzi anayefukuzwa kwa muda nje ya shule hapaswi kuadhibiwa mara mbili kwa kosa lilelile. Ikiwa safari za kwenda uwandani, mikusanyiko, au shughuli nyingine yoyote inatokea wakati mwanafunzi anatumikia adhabu yake ya kufukuzwa kwa muda nje ya shule, anaweza asihudhurie tukio hilo, hata hivyo, endapo tukio litatokea nje ya muda ambao mwanafunzi huyo anatumikia adhabu yake ya kufukuzwa nje ya shule, hapaswi kuondolewa kwenye tukio hilo isipokuwa kama kuna wasiwasi wa usalama.

Vitendo vya Kiwango cha 3 ni vya uzito mkubwa na, vinapotokea, vinaweza kutarajiwa kuwa na tishio kwenye afya, usalama au mali ya mtu yeyote. Msimamizi anaarifiwa pale ambapo kitendo cha Kiwango

cha 3 kinatokea. Wanafunzi wanaweza kufukuzwa shule kwa ajili ya vitendo vya Kiwango cha 3. Wasimamizi wa shule wanatakiwa kushauriana na Warakibu wao Wasaidizi kabla ya kuendelea kesi ya Shambulio, Shambulio Kubwa, au Silaha. Vitendo vyenye alama ya nyota vinaanzisha arifa ya lazima kwenye polisi ya shule kwa mujibu wa Kifungu cha Kanuni ya Shule 1303-A(b) na 22 Pa. Kifungu cha Kanuni 10.22.

***302.A. Uharibifu au Uporaji wa Mali ya Shule (Vurugu)**: Mwanafunzi hatakusudia kusababisha au kujaribu kusababisha uharibifu kwenye jengo la shule au kuiba au kujaribu kuiba mali ya shule. Uharibifu, au wizi katika kiwango hiki cha kosa, unazidi doma mia moja (USD 100).

***302.B. Uharibifu au Uporaji wa Mali Binafsi**: Mwanafunzi hatakusudia kusababisha au kujaribu kusababisha uharibifu mkubwa kwenye jengo binafsi au kuiba au kujaribu kuiba mali binafsi. Mali binafsi za thamani hazipaswi kuletwa shuleni. Uharibifu, au wizi katika kiwango hiki cha kosa, unazidi doma mia moja (USD 100).

***307. Dawa za Kulevya Ikiwa ni Pamoja na Makosa Yasiyo Makubwa Sana ya Bange, Paraphernalia, na Pombe:** Mwanafunzi hatamiliki, kutumia, kusambaza au kuwa chini ya ushawishi wa kilevi cha aina yoyote. Hata hivyo, katika jitihada za kupunguza adhabu kali, mwitikio stahiki wa kushughulikia dawa za kulevya kulinga na ukubwa wa kosa umeelezewa kulingana na aina ya kosa la dawa kwenye ukurasa wa [PLACEHOLDER #]. Ukiukaji wa Kanuni ya 307 unajumuisha makosa ya mara ya kwanza ya bange chini ya gramu 5, pombe na kumiliki paraphenalia yakitokea katika mwaka wa masomo uleule. Tafadhali kumbuka kwamba matumizi ya dawa iliyoudhinishwa na daktari aliyesajiliwa kwa mwanafunzi ambaye amenadikiwa hakutachukuiwa kuwa ni ukiukaji wa kanuni hii, lakini unaweza kuwa ni ukiukaji wa Sera ya Wilaya ya Matumizi ya Dawa.
Kushindwa kuzingatia sera ya Matumizi ya Dawa kunaweza kusababisha pia kupewa adhabu shuleni.

313. Unyanyasaji: Aina ya ubaguzi kulingana na mbari, rangi, umri, kabila, dini, jinsi, jinsia (ikiwa ni pamoja na utambulisho wa kijinsia), mwelekeo wa kingono, asili, asili ya taifa, hali ya ndoa ujauzito au ulemavu ikiwa ni pamoja na vitendo visisvyotakiwa, au vitendo vingine ambavyo vinaweza kuwa na madhara au vya kudhalilisha au kuingilia shule ya mtu au utendaji unaohusiana na shule pale ambapo kitendo hicho ni kibaya, kinadumu au kinapotosha na mtu wa kawaida katika sehemu ya mlalamikaji anaweza kuona kwamba inaweka mazingira ya kielimu ya kuogopesha, kutisha au kunyanyasa.

Unyanyasaji unajumuisha kosa la Kiwango cha 3, tofauti na Kiwango cha 2, ambapo kitendo hicho ni kibaya sana, cha hatari, au haramu kiasi kwamba Wilaya haiwezi kurarajia inaweza kusahihisha kikamilifu kupitia uingiliaji kati.

Vitendo mahususi vya unyanyasaji vimefafanuliwa zaidi kama ifuatavyo:

***313.A. Unyanyasaji wa Kingono:** Kitendo cha kingono ambacho hakijakubaliwa na kinachukuliwa na mtu wa kawaida kuwa ni kibaya, kilichopotoka na cha uhalifu ambacho kinamnyima mtu husika ufikiaji sawa wa mpango wa Wilaya. Unyanyasaji wa kingono kwa madhumuni ya kupewa upendeleo, kumhitaji mtu atoe ndono bila ridhaa yake kwa lengo la kupewa msaada, manufaa au huduma pia unashughulikiwa na sera ya Wilaya. Ukatili wa kingono, ukatili kwenye mahusiano, ukatili wa nyumbani na kumfuatilia mtu, kama ilivyofafanuliwa kwenye sera ya Wilaya pia ni aina ya unyanyasaji wa kingono.

313.B. Unyanyasaji wa Kimbari/Kabila Ubaguzi kwa msingi wa mbari, rangi au asili ya utaifa, ikiwa ni pamoja na ubaguzi kwa msingi wa mbari halisi ya mtu au inayodhaniwa, rangi, asili ya kitaifa, kabila au ukoo. Hii inajumuisha ubaguzi kwa msingi wa nchi, dunia, au eneo, ambapo mtu au mababu zake wanatoka huko; mtu kutozungumza Kiingereza au hali ya Mjifunzaji wa Kiingereza; au asili halisi ya mtu au

inayodhaniwa au sifa za kikabila, ikiwa ni pamoja na ushiriki katika dini ambayo inaweza kudhaniwa kuwa inaonyesha tabia hizo (kama vile, Wahindu, Wayahudi< Waislamu na Wasikh).

313.C. Unyanyasaji wa Kijinsia: Unaweza kujumuisha vitendo maneno, visivyo vya maneno au vya kimwili vinavyoogopesha au vinavyojenga chuki kwa sababu ya mitazamo ya kijinsia. Kwa hivyo, unyanyasaji wa mwanafunzi kushindwa kufuata dhana za kibaguzi za uanaume na uanamke unajumuisha ubaguzi wa kijinsia. Unyanyasaji wa kijinsia unaweza kutokwa kwa kukiuka sera ya Wiliaya na/au Sura ya IX wakati kitendo hicho kinamnyima au kinazuia uwezo wa mwanafunzi kupokea msaada wa kieleimu, manufaa, huduma au kutendewa.

313.D. Unyanyasaji kutokana na Ulemavu Tabia za kuogopesha au unyanyasaji kwa mwanafunzi kwa msingi wa ulemavu ambao unatengeneza mazingira ya uadui kwa kuingiliana na au kumnyima mwanafunzi kushiriki au kupokea manufaa, huduma au fursa katika mpango wa taasisi. Matendo ya unyanyasaji yanaweza kujumuisha vitendo vya kutamka na matusi, vilevile tabia isiyo ya maneno kama vile kauli za grafiki na za maandishi au matendo ambayo yanatishia kimwili, yenye madhara, au yanadhalilisha.

313.E. Aina nyingine ya Unyanyasaji: Kitendo chochote ambacho kinakiuka Katazo la Wilaya la Sera ya Uchokozi/Unyanyasaji ambayo haikidhi fasili ya unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kimbari/kikabila, unyanyasaji wa kijinsia au unyanyasaji kutokana na ulemavu.

314. Kutumia Vibaya Kompyuta/Mitandao ya Kompyuta/Kifaa cha Kielektroniki:: Mwanafunzi hatajihusisha na kitendo chochote kinchokiuka Sera ya Wilaya ya Matumizi ya Mtandao na Usalama, miongozo yoyote ya matumizi ya kompyuta ya shule au miongozo ya matumizi ya kifaa cha mkononi, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu vitendo vifuatavyo na vifaa vya watu wengine:

A. Barua pepe za chuki, maoni ya kibaguzi, vilevile mawasiliano ya kuudhi ambayo hayaweki hatari kwenye usalama
B. Kutumia kifaa chochote cha kielektroniki kuonyesha au kufikia picha za utupu au nyenzo za ponografia
C. Usambazaji wa lugha au picha za kingono, ikiwa ni pamoja na picha za mtu husika
D. Uharibifu, urekebishaji au matumizi mabaya ya maunzi ya mtandao, programu au maarifa
E. Kuchukua video za ugomvi au kuchukua video za mtu ambaye yupo katika sehemu ambapo anatarajia kuwa na faragha
F. Kuchapisha video ya kitendo cha mwanafunzi kwenye mtandao wa kijamii ambayo inaathiri jumuiya ya wanafunzi au watu walio katika jumuiya ya shule katika njia mbaya.

Ustaarabu mzuri katika matumizi ya mtandao utafundishwa na kutekelezwa kabla ya kuendelea na kutoa adhabu kwa ajili ya ukiukaji wa matumizi sahihi ya kompyuta.

317.A. Uchokozi: Uchokozi humaanisha kitendo cha kukusudia kupitia elektroniki, maandishi, maneno au kitendo halisi au mfululizo wa vitendo vinavyoelekezwa kwa mwanafunzi au wanafunzi wangine, ambacho kinatokea katika mazingira ya shule, ambacho ni kibaya sana, cha kuendelea au kupotosha chenye kusudi au nia ya:

1. Kuunda mazingira ya kuogopesha au ya chuki ambayo hatimaye yanaingiliana na elimu ya mwanafunzi au
2. Kumdhuru mwanafunzi, kimwili, kihisia au kiakili; au
3. Kumweka mwanafunzi katika hofu dhahiri ya madhara ya kimwili au kihisia; au
4. Kumweka mwanafunzi katika hofu dhahiri ya kuharibu au kupoteza mali binafsi ya mtu

317. **B. Uchokozi wa mtandaoni**: Uchokozi hujumuisha uchokozi wa mtandaoni na/au uchokozi kupitia vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, mitandao ya kijamii, barua pepe, ujumbe wa papo hapo, ujumbe wa maandishi, ujumbe wa Twitter (kwenye Twitter), blogi, kushiriki picha na video, vyumba vya kuchati, dashibodi au tovuti. Uchokozi unaweza kujumuisha vitendo ambavyo ninatokea nje ya shule ikiwa vigezo kadhaa vinakidhiwa. Katazo kamili la Sera ya Uchokozi/Unyanyasaji, malalamiko na taratibu za uchunguzi unachaposhwa kwenye tovuti ya Wilaya kupitia www.pps.k12.pa.us/Page/481, na katika kila jengo na darasa.

318. **Udhalilishaji:** Udhalilishaji unatokea pale ambapo mtu kwa kukusudia, kwa kujua au bila kujali, kwa kusudi la kuanzisha, kuingia au kumshirikisha mwanafunzi kwenye kikundi kwa kusudi la kuendelea au kuimarisha uanachama au hali katika kikundi, anasababisha au kumlazimisha mwanafunzi afanye yoyote kati ya haya yafuatayo:

1. Kukiuka sheria ya shirikisho au jimbo.
2. Kula chakula chochote, kimiminika, kimiminika cha pombe, dawa za kulevya au dutu nyingine yoyote ambayo inamweka mwanafunzi kwenye hatari ya madhara ya kihisia au kimwili.
3. Kustahimili ukatili wa asili ya kiakili, ikiwa ni pamoja na shughuli inayoathiri kwa kiasi kikubwa afya ya akili au utu wa mtu, kukosa usingizi, kujiondoa katika mikusanyiko ya kijamii au kitendo ambacho kinaweza kusababisha fadhaa kubwa.
4. Kustahimili ukatili wenye asili ya kingono.
5. Kustahimili shughuli nyingine yoyote ambayo inaunda uwezekano wa madhara ya kimwili kwa mwanafunzi.

Shughuli yoyote, kama ilivyoelezwa hapo juu, itachukuliwa kuwa ni ukiukaji bila kujali endapo idhini ya mwanafunzi ilitolewa au la.

321. **Vitisho vya Kigaidi**. Tishio linalowasilishwa ama moja kwa moja au isivyo moja kwa moja ili kufanya uhalifu wowote wa ukatili kwa nia ya kumtia hofu mtu mwingine, kusababisha ufurushwaji kwenye jengo, sehemu ya mkusanyiko au kwenye usafiri wa umma; au vinginevyo kusababisha usumbufu mkubwa katika umma, au kusababisha hofu au usumbufu mkubwa katika umma kwa kupuuzia hatari ya kusababisha hofu kubwa au usumbufu.

322. **Kitendo cha Kingono/Ukosefu wa Maadili:** Matendo ya kingono katika kiwango hiki cha kosa hujumuisha kujihusisha katika ngono, ngono ya mdomoni vitendo vya kingono katika viwanja vya shule.

***323.** **Kuchochea Usumbufu au Vurumai**: Kusababisha usumbufu mkubwa au ugomvi miongoni mwa kikundi cha watu, ikisababisha uingiliaji kati wa wafanyakazi kadhaa wa shule na mfanyakazi wa usalama wa shule ili kutuliza usumbufu huo.

***326.A.** **Wizi, Udokozi, au Ujambazi kwenye Majengo ya Shule**: Mwanafunzi haruhusiwi kuiba au kujaribu kuiba au kufanya uvamizi kwenye jengo la shule. Wezi, udokozi au ujambazi katika kiwango hiki cha makosa kinazidi USD 100.

***326.B.** **Wizi, Udokozi au Ujambazi kwenye Majengo Binafsi:** Mwanafunzi haruhusiwi kuiba au kujaribu kumwimbia mwanafunzi mwingine au kufanya uvamizi kwenye jengo binafsi. Wezi, udokozi au ujambazi katika kiwango hiki cha makosa kinazidi USD 100.

Kiwango cha 3 - Mifano ya Mwongozo wa Uingiliaji Kati
Orodha iliyo hapa chini imetolewa kama menyu ya machaguo yanayoweza kuwepo na haikusudiwi kutumika kwa mfuatano. Utekelezaji wa uingiliaji kati utakuwa mahususi, badala ya mbinu ya kipimo kimoja kinawatushea wote.

- Kutumia Mbinu za Urejeshaji (yaani, kauli zenye ufanisi, maswali ya kurejesha, vikundi mikutano isiyo rasmi maandalizi, mikutano rasmi ya urejeshaji, n.k.)
- Kuelekeza kwenye michakato ya Mifumo ya Usaidizi ya Ngazi Nyingi (MTSS)
- Kuelekeza kwenye mipango ya utatuzi wa migogoro ya shuleni (k.m mapatano ya kundi rika, mikutano ya urejeshaji)•
- Mkutano wa wanafunzi na walimu
- Mkutano wa wazazi au waliezi/walimu
- Kufunisha tena/kuunda matarajio
- Mkutano wa mwanafunzi/msimamizi
- Mkutano wa uingiliaji kati unaofanywa na mfanyakazi wa ushauri
- Kazi ya kutafakari ya maandishi
- Endeleza, hakiki, au pitia nyenzo binafsi za kupangaza mwanafunzi (k.m Mpango wa Usaidizi wa Tabia)
- Mabadiliko kwenye ratiba au darasa (kwa kumwarifu mzazi/ mlezi)
- Ushauri nasaha kwa mtu binafsi/kikundi
- Kuelekeza kwenye Mpango wa Usaidizi kwa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuiaji (k.m, mafunzo ya ujuzi wa mihemko ya uhusiano wa kijamii kama vile kudhibiti hasira, kuondoa matumizi ya nguvu, ujuzi wa kupangilia mambo) na/au uingiliaji kati (k.m ushauri nasaha wa mazoea ya kiafya)
- Mpango wa tabia ya mwanafunzi
- Kuelekezwa kwenye mpango ushauri mafunzo
- Kuelekezwa kwenye Shirika la Kijamii Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)
- Huduma ya jamii (kwa idhini ya mzazi)
- Mkataba usaidizi wa usimamizi wa tabia nzuri
- Uelekezaji wa tathmini ya pombe/dawa za kulevya
- Mbadala mwingine unaofaa wa hatua za kinidhamu za kipekee (hatua za kinidhamu za kipekee hujumuisha kukamwatwa, kufukuzwa kwa muda ndani ya shule, kufukuzwa kwa muda nje ya shule)

Mifano ya Hatua za Kinadhamu Zinazopendekezwa Pamoja na Miongozo ya Uingiliaji Kati Inayotumika (Kiwango cha 3)

- Kuzuiliwa safari za uwandani, mikusanyiko, au manufaa mengine maalumu
- Kufukuzwa kwenye shughuli za ziada
- Kusitishwa kupata manufaa ya usafiri
- Kusitishiwa kushiriki katika matukio maalumu au promosheni
- Kuelekeza na kushauriana na polisi ya shule kwa mujibu wa Sehemu Kanuni ya Shule 1303-A(b) na 22 Pa. Kifungu cha Kanuni 10.22
- Kufukuzwa shuleni kwa muda (Siku 4-10)

Mwanafunzi anayefukuzwa kwa muda nje ya shule hapaswi kuadhibiwa mara mbili kwa kosa lilelile. Ikiwa safari za kwenda uwandani, mikusanyiko, au shughuli nyingine yoyote inatokea wakati mwanafunzi anatumikia adhabu yake ya kufukuzwa kwa muda nje ya shule, anaweza asihudhurie tukio hilo, hata hivyo, endapo tukio litatokea nje ya muda ambao mwanafunzi huyo anatumikia adhabu yake ya kufukuzwa nje ya shule, hapaswi kuondolewa kwenye tukio hilo isipokuwa kama kuna wasiwasi wa usalama.

Vitendo vya Kiwango cha 4 ni vya uzito mkubwa na vinaweza kuwa na tishio kwenye afya, usalama au mali ya mtu yeyote. Msimamizi anapaswa ataarifiwe wakati ambapo Kiwango cha 4 cha kitendo kimetokea, kwa njia ya kurejelea adhabu au kauli ikielezea tukio. Wanafunzi wanaweza kusimamishwa masomo ya kufukuzwa shule kwa ajili ya vitendo vya Kiwango cha 4. Wasimamizi wa shule wanatakiwa

kushauriana na Warakibu wao Wasaidizi kabla ya kuendelea kesi ya Shambulio, Shambulio Kubwa, au Silaha. Vitendo vyenye alama ya nyota vinaanzisha arifa ya lazima kwenye polisi ya shule kwa mujibu wa Kifungu cha Kanuni ya Shule 1303-A(b) na 22 Pa. Kifungu cha Kanuni 10.22.

404. Kumshambulia Mfanyakazi wa Shule: Mwanafunzi anapojihusisha kwenye vitendo vyovyote kati ya hivi vifuatavyo dhidi ya mwajiriwa wa shule au mkandarasi: (1) kujaribu kusababisha au kwa makusudi, kwa kujua au bila kujali kusababisha majeraha ya mwili kwa mfanyakazi wa shule bila maneno ya kuchochea hasira; (2) kusababisha jeraha la kimwili kwa mtu mwingine kwa kuzembea kwa salaha mbaya; au (3) kujaribu kusababisha hatari ya kimwili kumweka mwingine katika hofu hatari kubwa ya kusababisha jeraha la kimwili.

405.A. Mashambulizi kwa Mwanafunzi au Mtu Mwingine Ambaye Si Mwajiriwa wa Shule: Pale ambapo mwanafunzi kwa kukusudia na bila maneno ya kusababisha hasira anampiga, anampiga ngumu au anampiga mateke mwanafunzi au mtu mwingine aliyeajiriwa na shule. Matendo mengine ya kimwili ambayo hayakidhi fasili ya mashambulizi yanaweza kuangukia katika katazo dhidi ya kupigana, uchokozi na/au unyanyasaji.

***405.B. Mashambulizi Makubwa kwa Mwanafunzi au Mtu Mwingine Ambaye Si Mwajiriwa wa Shule.** Mwanafunzi
(1) atakapojaribu kusababisha majeraha makubwa ya kimwili kwa mwingine, au kusababisha jeraha hilo kwa kukusudia, kwa kujua au kwa kutojali katika mazingira ya kudhihirisha kutojali kwa hali ya juu kuhusu maisha ya binadamu; au (2) kujaribu kusababisha au kwa kukusudia au kwa kujua kusababisha jeraha la kimwili kwa miwngine kwa kutumia silaha kali.

***406. Silaha na Vifaa vya Hatari:** Mwanafunzi hatamiliki, kushika au kuhamisha kitu chochote kilichofasiliwa na Kanuni ya Shule ya Pennsylvania kuwa ni silaha (hapa ikirejelewa kama “silaha”) akiwa katika jengo lolote la shule, akiwa katika shughuli yoyote iliyofadhiliwa au kuidhinishwa na shule au akitembea au akisafirishwa kwa namna yoyote kwenda au kutoka shuleni au kwenye shuguli iliyofadhiliwa au kuidhinishwa na shule.

a. **Silaha kama Zinavyofasiliwa na Sheria.** Neno “silaha,” kwenye Kanuni ya Shule, hujumuisha lakini si tu kisu, kifaa cha kukatia, zana ya kukatia, kilipuzi, nunchaku, silaha ya moto, pisto, gobole, na/au nyenzo nyingine yoyote, kifaa au kitu chenye uwezo wa kusababisha majeraha makubwa ya kimwili. Wakati wa kuamua iwapo kitu fulani ni silaha, shule inapaswa kuangalia kitu hicho kwa kawaida kinakusudiwa kufanya nini. Namna ambavyo mwanafunzi anatumia kitu hakufanyi kigeuzwe kuwa silaha.

b. **Vitu vya Kujilinda.** Kitu cha kujilinda ni zana, kifaa au kitu ambacho kimetengenezwa kwa ajili ya au kwa kawaida kinatumiwa kwa ajili ya kujilinda. Mifano inajumuisha lakini si tu pilipili ya kupuliza, minyororo ya kujilinda , pete za kujilinda, kalamu za kiufundi au tochi na kubatoni. PPS itamshitaki tu mwanafunzi kwa ukiukaji wa matumizi ya silaha ikiwa mwanafunzi huyo ametumia au ametishia kutumia kitu cha kujilinda dhidi ya mtu mwingine.

c. **Kitu kinachofanana.** Mfanano wowote wa kisu, kifaa au nyenzo ya kukatia, nunchaku, silaha ya moto, pisto au gobole. Wakati wanafunzi wanaweza kufikia vitu vinavyofanana ambavyo vinauzwa kama midoli au mavazi ya sanaa, vitu hivyo vinakatazwa katika mazingira ya shule au katika matukio yaliyofadhiliwa na shule. Watu wanaokuja na vitu vinavyofanana vitapokonywa na hawatapokea adhabu isipokuwa kifaa hicho kilitumiwa kufanya vitendo fulani ambavyo vimekatazwa na kanuni hii ya Kanuni ya Maadili ya Wanafunzi.

***407. Kumiliki, Kutumia au Chini ya Ushawishi wa Pombe au Dawa za Kulevya:** Wanafunzi walio na kiasi kikubwa cha dawa (yaani, zaidi ya gramu 5 za bange); dawa za kulevya zilizofasiliwa katika Viambatisho I hadi V vya Sheria ya Dutu Zinazodhibitiwa[1], yaani, Adderall; na makosa ya kujirudia ya dawa za kulevya yanachukuliwa kuwa ukiukaji wa Kiwango cha 4. Mwanafunzi hatamiliki, kutumia, kusambaza au kuwa chini ya ushawishi wa kilevi cha aina yoyote.
Hata hivyo, katika jitihada za kupunguza adhabu kali, mwitikio stahiki wa kushughulikia dawa za kulevya au pombe kulinga na ukubwa wa kosa umeelezewa kulingana na aina ya kosa la dawa kwenye kurasa zinazofuata Hii inajumuisha dawa zote za kulevya; viwango vya juu vya dawa za kulevya vinavyokidhi vikomo kusudi la kusambaza; kiwango cha bangi gramu 5 au zaidi ya gramu 5 na uhalifu unaojirudia wa bange na pombe unaotokea katika mwaka uleule wa masomo.

Tafadhali kumbuka kwamba matumizi ya dawa iliyoudhinishwa na daktari aliyesajiliwa kwa mwanafunzi ambaye amenadikiwa hakutachukuiwa kuwa ni ukiukaji wa kanuni hii, lakini unaweza kuwa ni ukiukaji wa Sera ya Matumizi ya Dawa. Kushindwa kuzingatia sera ya Matumizi ya Dawa kunaweza kusababisha pia kupewa adhabu shuleni.

Kama sehemu ya jitihada za Wilaya kuendelea kubadilisha mchakato wa kupunguza adhabu ya kipekee, mchakato wa ngazi ya juu kwa ajili ya mwitikio wa kiusimamizi kwenye ukuikaji wa dawa za kulevya na pombe umetumika.

Fasili zinazofaa chati ya mwitikio wa ngazi ya juu hapa chini zipo kwenye ukurasa unaofuata.

- Dawa za kulevya: Mihadarati yoyote, dawa zozote za kupumbaza akili, amphetamine, barbiturate dawa zingine za kulevya zinazosababisha kubadilisha akili au athari za kilevi, dawa za kulevya za mbunifu, au dutu nyingine yoyote inayodhibitiwa, kama ilivyofasiliwa kwenye Kiambatisho I hadi cha V vya Sheria ya Dutu Zinazodhibitiwa (21 U.S.C. § 812) zimefasiliwa zaidi na kanuni kwenye 21 C.F.R. Sehemu 1308.11 hadi 1308.15, au kama ilivyofasiliwa kwenye Sheria ya Dutu, Dawa, Vifaa na Vipodozi Vinavyodhibitiwa (35 P.S. §780-101), Sheria ya Pennsylvania ya Matumizi Mabaya ya Dawa za Kulevya na Pombe (71 P.S. §1690.101), (kwa pamoja “Sheria”) au kanuni yoyote inayohusiana na Sheria au kanuni au utaratibu wowote wa kurithi.
- [1] Sheria ya Dutu Zinazodhibitiwa (21 U.S.C. § 812) na imefasiliwa zaidi kwenye kanuni katika 21 C.F.R. Sehemu 1308.11 hadi 1308.15, au kama inavyofafanuliwa katika Sheria ya Udhibiti wa Dutu, Dawa za Kulevya, Vifaa na Vipodozi (35 PS § 780-101), Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Pombe ya Pennsylvania (71 PS §1690.101), (kwa pamoja “Vitendo”) au kanuni zozote zinazohusiana na Matendo, au sheria au kanuni yoyote ya mrithi.
- Bangi: Inarejelea bangi, mafuta ya THC, au aina yoyote ya vitu hivi kwa namna yoyote, ikiwa ni pamoja na lakini si tu, yenye nta, vyakula, vidonge, mafuta, mapovu kama vile, krimu au marashi, mapovu yanayotolewa kama mvuke au nebula, tinkcha, au kioevu.
- Pombe: Kinywaji chochote cha pombe, kinywaji cha malta, divai iliyoboreshwa, au kileo kingine.•
- Paraphernalia: Karatasi za kusokotwa, klipu za roach, hemostats, mabomba au sehemu za mabomba, na vifaa vingine vilivyotengenezwa nyumbani vinavyotumiwa kumeza dawa.
- Mabaki ya Dawa: Kiasi kidogo cha dawa ambayo inabaki baada ya uwepo mkubwa wa dutu hiyo kutumiwa au kuondolewa (kwa mfano, resini ambayo ni bidhaa ya bangi iliyovutwa).
- Kosa la Kujirudia la Kuvuta Sigara na Pombe: Kosa la pili au la baadaye la dawa za kulevya na pombe katika mwaka huo huo wa masomo. Jumla ya makosa katika mwaka mmoja wa masomo yatajumuisha makosa kutoka shule za awali ambazo mwanafunzi aliandikishwa. Mwanafunzi

anapokuwa na zaidi ya kosa moja la dawa za kulevya na pombe katika mwaka fulani wa masomo, kosa lolote la dawa za kulevya na pombe katika mwaka unaofuata wa masomo linachukuliwa kuwa kosa la kurudia.

- Programu ya ATOD: Mpango wa Pombe, Tumbaku, na Matumizi Mengine ya Dawa Yasiyo Sahihi IAES: Mpangilio wa Elimu Mbadala ya Muda

Aina za Uhalifu wa Dawa za Kulevya na Muundo wa Mwitikio

Chati ya Muundo wa Majibu iliyo hapa chini inatumika kwa wanafunzi wa elimu ya kawaida ambao hawastahiki kupata huduma za IEP. Muundo wa mwitikio uliopendekezwa kwa wanafunzi wenye ulemavu wanaostahiki IEP zimebainishwa katika italiki ndani ya Chati ya Muundo wa Mwitikio. Wanafunzi wenye Mipango 504 na wanafunzi ambao Wilaya inatarajiwa kuwa na ufahamu kuhusu ulemavu wa mwanafunzi (yaani, "wanaofikiriwa kuwa"), wana haki ya kupata ulinzi sawa wa kinidhamu kama ule wanaopewa wanafunzi walio na IEPs. Ingawa nafasi ya siku 45 kwa ukiukaji mkubwa haipatikani kiotomatiki kwa mwanafunzi aliye na Mpango wa 504, Timu ya 504 ya wanafunzi, pamoja na Mzazi/Mlezi, inaweza kukubali kwamba nafasi ya siku 45 inafaa, maadamu huduma katika Mpango wa 504 wa mwanafunzi zinaweza kutekelezwa kwa ufanisi katika mazingira mbadala. Shule zinaelekezwa kushauriana na Ofisi ya Huduma za Usaidizi kwa Wanafunzi na Idara ya Sheria kwa ajili ya mwongozo.

Mifumo iliyoainishwa ya muda wa kusimamishwa masomo kwa ajili ya ukiukaji wa Ngazi ya 3/Kanuni ya 307 inaweza kupunguzwa wakati wa kushughulikia programu ya Pombe, Tumbaku, na Dawa Zingine (ATOD). Kwa umahususi, mwanafunzi atatumikia siku tano (5) za kipindi cha kusimamishwa masomo (siku mbili (2) kwa wanafunzi walio na IEP) na siku zilizobaki zitafanyika kwa utulivu wakisubiri fursa ya kuhudhuria Programu ya ATOD kama ilivyoainishwa katika miongozo hii.

Wanafunzi hawatamiliki, kutumia, kusambaza, au kuwa chini ya ushawishi wa dutu yoyote inayodhibitiwa, pamoja na bangi. PPS inatambua kwamba bangi inapatikana kwa urahisi zaidi kwa madhumuni ya matibabu kama matokeo ya Sheria ya jimbo ya Bangi ya Matibabu, 35 Pa. C.S. § 10231.101, na kadhalika. Hata hivyo, bangi inabaki kuwa dutu haramu kwa mujibu wa sheria za shirikisho. Jimbo la Pennsylvania kuhalalisha bangi kwa madhumuni ya matibabu hakuchukui utekelezaji wa sheria za shirikisho za dawa za kulevya, pamoja na zile ambazo zinakataza uwepo na matumizi ya dawa za kulevya kwenye jengo la shule, pamoja na Sheria ya Kila Mwanafunzi Anafanikiwa, 20 U.S.C. § 71118. Umiliki wa bangi ni kosa la jinai chini ya sheria za Jimbo na Shirikisho na pia ni ukiukaji wa Sera ya Wilaya 217 – Dawa za Kulevya na Pombe: https://go.boarddocs.com/pa/pghboe/Board.nsf/Public#.

Marufuku ya bangi kwa misingi ya shule inahusu bangi, THC, au THC kwa namna yoyote, ikiwa ni pamoja na bidhaa za bangi. Aina zilizopigwa marufuku za bangi zinahusu vitu hivi kwa aina yoyote, ikiwa ni pamoja na lakini si tu, nta, vyakula, vidonge, mafuta, mapovu kama vile jeli, krimu au marashi, uturi, fomu za maua au vikonyo, na mapovu yanayotolewa kwa mvuke au nebula, tincture, au kioevu. PPS itazingatia mwongozo wowote wa serikali au shirikisho ambao unaweza kutolewa kuhusiana na umiliki wa bangi au bidhaa za bangi kwenye maeneo ya shule.

Wanafunzi wanaopatikana kuwa na chini ya gramu 5 za bangi kwenye kosa la FIRS wanatajwa kuwa wanakiuka Kanuni za Maadili 307. Wanafunzi walio na gramu 5 au zaidi ya bangi, au kosa la pili kwa kuwa na chini ya gramu 5, wataelekezwa kwenye ukiukaji wa Kanuni za Maadili 407. Wanafunzi ambao wanawasilisha dawa ya bangi ya matibabu, kadi au vyeti vinavyoidhinisha matumizi ya hali yao ya

matibabu hawatapokea matokeo yoyote ya nidhamu kwa kumiliki au kutumia bangi kwa sababu za shule . Hata hivyo, vitu vyote vinavyodhibitiwa, ikiwa ni pamoja na bangi, vitapokonywa na utawala wa shule na kuwekwa chini ya uangalizi wa Idara ya Usalama wa Shule.

Kosa la Dawa za Kulevya Aina	Kiwango cha 3 Kusimamishwa kwa siku 10 *Kusimamishwa kwa siku-3**	Kiwango cha 4 Kusimamishwa kwa Siku 10 + Kufukuzwa (Elimu Mbadala) *Kusimamishwa kwa Siku 3 + Nafasi ya Siku 45 Mpangilio wa Elimu Mbadala ya Mpito*
Paraphernalia (Kosa la Kwanza au Kurudia)	Umiliki wa paraphernalia kukiwa na bangi (mabaki au kiasi chini ya gramu 5)	Kurudia kosa la kumiliki paraphernalia na uwepo wa bangi (wingi) wowote
Aina ya Dawa: Pombe, Bangi, au Dawa Nyingine (Kosa la Kwanza au Kurudia)	Kosa la kwanza la umiliki wa pombe; Kosa la kwanza la umiliki wa bangi (mabaki au kiasi chini ya gramu 5)	Kurudia kosa la kumiliki pombe **; Kurudia kosa la umiliki bangi (kiasi chochote); Kosa la kwanza la umiliki wa bangi (gramu 5 au zaidi ya gramu 5); Umiliki wa dawa nyingine za kulevya tofuati na bangi
Nia ya Kusambaza		Umiliki wa bangi zaidi ya gramu 5 au gramu 5
Wngi	Umiliki wa bangi (mabaki au kiasi chini ya gramu 5)	Umiliki wa bangi gramu 5, zaidi ya gramu 5 au dawa nyingine yoyote au pombe

Ngazi ya Usaidizi	Aina ya Huduma kulingana na Kosa la Kanuni ya Maadili Kiwango	Mpango na Mtoa Huduma ***
Ngazi ya 3: Makosa ya Yanayofuata na/au Makali	Rufaa za Uchunguzi wa SAP Njia Mbadala ya Kusimamishwa Shuleni (ATOSS) Programu Madarasa na Huduma za Elimu ya Dawa za Kulevya (Ukiukaji wa Kanuni ya Maadili: Kiwango cha 4)	Kituo cha Mafanikio ya Wanafunzi ATOSS Programu/Nafasi ya Elimu Mbadala Watoa huduma wa SAP walioteuliwa (wanafunzi wanaweza kupokea huduma wakati wa kupata nafasi ya elimu mbadala) Matibabu ya Wagonjwa Wakaaji

Ngazi ya 2: Makosa Madogo ya Mara ya Kwanza	Rufaa za Uchunguzi wa SAP Njia Mbadala ya Kusimamishwa Shuleni (ATOSS) Programu (Ukiukaji wa Kanuni za Maadili: Kiwango cha 3)	FUKWE zilizoteuliwa za Watoa Huduma wa SAP Kituo cha Mafanikio ya Wanafunzi ATOSS Programu/Nafasi ya Elimu Mbadala Kituo kinachojali Programu ya ATOSS Mpango wa Elimu ya Dawa za Kulevya kwa Vijana ya Three Rivers
Ngazi ya 1: Kinga Majumui	Wazungumzaji wa Uhamasishaji na Elimu kuhusu Dawa za Kulevya	Allegheny Recovery Krew CVS Inashughulikia Uhamasishaji wa Dawa za Kulevya kuhusu dawa za opioid

- Wanafunzi wanapewa fursa ya kushikilia siku za kusimamishwa kwa mahudhurio na kufuata mpango wa ATOD.
- Tafadhali kumbuka: Wanafunzi walio na IEP wanaweza kuelekezwa kwenye IAES ya siku 45 kwa ajili ya kumiliki pombe au vifaa. Kwa wanafunzi walio na IEPs, neno "madawa ya kulevya" halijumuishi dutu inayodhibitiwa ambayo inamilikiwa kisheria au kutumika chini ya usimamizi wa mtaalamu wa huduma ya afya aliye na leseni au ambayo inamilikiwa kisheria au kutumika chini ya kifungu kingine chochote cha sheria ya shirikisho. Angalia 34 C.F.R. 300.530.
- Kwa kuwa programu inaweza kupanuliwa mwaka hadi mwaka, tafadhali tembelea tovuti ili upate tangazo la hivi karibuni zaidi. www.pghschools.org/conduct

Programu ya Pombe, Tumbaku na Dawa Zingine (ATOD)

Wilaya hutoa Mpango wa Utofauti wa Pombe, Tumbaku na Dawa Nyingine (ATOD) kwa wanafunzi ambao wamekiuka sheria za Kanuni ya Maadili ya Wanafunzi zinazohusiana na dawa za kulevya, pombe au uvutaji sigara. Wanafunzi wana siku tisini (90) kukamilisha saa tisa (9) za programu kwa njia ya mtandao. Wanafunzi lazima wakamilishe kozi zinazohitajika zilizotajwa hapo juu ndani ya siku 90 za kosa kwa ili siku za ziada za kusimamishwa zifanyike.

Mkuu wa shule au mtu maalumu anayeshughulikia nidhamu ya makosa ya dawa za kulevya na pombe atampa mwanafunzi na mzazi/mlezi nakala ya barua yenye taarifa za huduma za ATOD zilizosasishwa zaidi ikiwa na barua ya awali ya Kusimamishwa. Barua ya habari kuhusu huduma na usaidizi wa ATOD itaelezea tarehe, nyakati, na maeneo ya huduma zote za Programu ya ATOD na usaidizi.

Huduma na usaidizi wa ATOD pia zinaweza kutumika kwa ufanisi kwa ajili ya wanafunzi. Kwa mfano, ikiwa mwanafunzi atakutwa kuwa na kiwango cha juu au harufu ya bangi.

Kwa wanafunzi ambao wamefungwa kwa sababu ya kosa lao la kukiuka Kanuni za Maadili kwa mujibu wa sheria utekelezaji, kufukuzwa shuleni hakutaanza kutekelezwa hadi mwanafunzi aachiliwe huru. Vivyo hivyo, ratiba ya siku 60 za kukamilika kwa Programu ya ATOD haitaanza hadi mwanafunzi aachiliwe kutoka kizuizini.

Ushirikishwaji wa Utekelezaji wa Sheria na Vitu vya Upimaji

Mwanafunzi anapokutwa na dawa za kulevya au pombe kama ilivyopigwa marufuku na Sera ya Bodi, Idara ya Usalama wa Shule itaarifiwa kuhusu ukiukaji huo bila kuchelewa. Ushahidi unaofaa uhifadhi na mlolongo wa taratibu za utunzaji wa Idara ya Usalama wa Shule utafuatwa. Idara iliyokabidhiwa ya Afisa wa Polisi wa Shule wa Usalama itawajibika kwa ufungaji wa dutu au bidhaa iliyokatazwa. Upimaji wa awali wa dawa zilizopigwa marufuku au mabaki ni jukumu la Afisa wa Polisi wa Shule aliyeteuliwa. Dutu hiyo itatolewa kwa Maabara ya Uhalifu ya Kaunti ya Allegheny kwa ajilio ya upimaji na uzani zaidi. Ripoti ya siri ya Matokeo ya Maabara na Ripoti ya Kitengo cha Kemia ya Dawa kisha hutolewa kwa Idara ya Usalama wa Shule. Ripoti za Maabara ya Uhalifu kisha zitatolewa kwa Ofisi ya Huduma za Usaidizi wa Wanafunzi.

Kumiliki kalamu ya mvuke iliyo na mafuta ya THC ni ukiukaji wa sera ya Wilaya ya madawa ya kulevya na pombe. Vitu vilivyomo kwenye kalamu za mvuke yatajaribiwa ili kubaini ikiwa dutu hiyo ni mafuta ya THC. Wanafunzi ambao wana kalamu moja au mbili za mvuke zilizo na THC watashughulikiwa chini ya Kanuni ya 307. Umiliki wa kalamu tatu (3) au zaidi za mvuke zilizo na THC utashughulikiwa chini ya Kanuni ya 407. Ukiukaji wa mara kwa mara wa kalamu ya mvuke pia utashughulikiwa chini ya Kanuni ya 407.

408. ***Uhalifu wa Kuchoma Moto*****:** Kuanzisha moto au mlipuko kwa makusudi, au kusaidia, kuuliza, au kumwambia mtu mwingine, kuwasha moto au mlipuko, ambao unaweza au unaweka mali katika hatari ya kuharibiwa au mtu (pamoja na mzima moto) katika hatari ya kuumia.

418. ***Uharibifu Uliokithiri*** Hutokea wakati mtu anapofanya kitendo cha uharibifu kama ilivyofafanuliwa na Kanuni ya 218 au 318 ambayo husababisha jeraha kubwa la mwili au kifo kwa mwanafunzi na:

1. Mwanafunzi hutenda kwa kutojali afya na usalama wa mwanafunzi mwathiriwa; au
2. Mwanafunzi husababisha, kulazimisha matumizi ya kioevu cha pombe au dawa ya kulevya kwa mwanafunzi aliyeathiriwa.

Wasimamizi wa shule wanashauriwa kushauriana na Ofisi ya Huduma za Usaidizi kwa Wanafunzi kabla ya kumshtaki mwanafunzi kwa ukiukaji wa Shambulio au Silaha.

Kiwango cha 4 - Mifano ya Mwongozo wa Uingiliaji Kati *Orodha iliyo hapa chini imetolewa kama menyu ya machaguo yanayoweza kuwepo na haikusudiwi kutumika kwa mfuatano. Utekelezaji wa uingiliaji kati utakuwa mahususi, badala ya mbinu ya kipimo kimoja kinawatushea wote.*
• Kutumia Mbinu za Urejeshaji (yaani, kauli zenye ufanisi, maswali ya kurejesha, vikundi mikutano isiyo rasmi maandalizi, mikutano rasmi ya urejeshaji, n.k.) • Kuelekeza kwenye michakato ya Mifumo ya Usaidizi ya Ngazi Nyingi (MTSS) • Kuelekeza kwenye mipango ya utatuzi wa migogoro ya shuleni (k.m mapatano ya kundi rika, mikutano ya urejeshaji) • Mkutano wa Wanafunzi/Walimu • Mkutano wa wazazi au waliezi/walimu • Mkutano wa mwanafunzi/msimamizi • Mkutano wa uingiliaji kati unaofanywa na mfanyakazi wa ushauri • Kazi ya kutafakari ya maandishi • Endeleza, hakiki, au pitia nyenzo binafsi za kupangaza mwanafunzi (k.m Mpango wa Usaidizi wa Tabia)

- Mabadiliko kwenye ratiba au darasa (kwa kumwarifu mzazi/ mlezi)

- Ushauri nasaha kwa mtu binafsi/kikundi
- Kuelekeza kwenye Mpango wa Usaidizi kwa Wanafunzi (SAP) kwa ajili ya uzuiaji (k.m, mafunzo ya ujuzi wa mihemko ya uhusiano wa kijamii kama vile kudhibiti hasira, kuondoa matumizi ya nguvu, ujuzi wa kupangilia mambo) na/au uingiliaji kati (k.m ushauri nasaha wa mazoea ya kiafya)
- Mpango wa tabia ya mwanafunzi
- Kuelekezwa kwenye mpango ushauri mafunzo
- Kuelekezwa kwenye Shirika la Kijamii Lililoidhinishwa na Wilaya (CBO)
- Huduma ya jamii (kwa idhini ya mzazi)
- Mkataba usaidizi wa usimamizi wa tabia nzuri
- Uelekezaji wa tathmini ya pombe/dawa za kulevya
- Mbadala mwingine unaofaa wa hatua za kinidhamu za kipekee (hatua za kinidhamu za kipekee hujumuisha kukamwatwa, kufukuzwa kwa muda ndani ya shule, kufukuzwa kwa muda nje ya shule)

Mifano ya Hatua za Kinidhamu Zinazopendekezwa Pamoja na Miongozo ya Uingiliaji Kati Inayotumika (Kiwango cha 4)

- Kuzuiliwa safari za uwandani, mikusanyiko, au manufaa mengine maalumu
- Kufukuzwa kwenye shughuli za ziada
- Kusitishwa kupata manufaa ya usafiri
- Kusitishiwa kushiriki katika matukio maalumu au promosheni.
- Kuelekeza na kushauriana na polisi ya shule kwa mujibu wa Sehemu Kanuni ya Shule 1303-A(b) na 22 Pa. Kifungu cha Kanuni 10.22.
- Kufukuzwa shuleni kwa muda
- Kutengwa/kufukuzwa (siku 11 au zaidi)
- Nafasi ya elimu mbadala

Mwanafunzi anayefukuzwa kwa muda nje ya shule hapaswi kuadhibiwa mara mbili kwa kosa lilelile. Ikiwa safari za kwenda uwandani, mikusanyiko, au shughuli nyingine yoyote inatokea wakati mwanafunzi anatumikia adhabu yake ya kufukuzwa kwa muda nje ya shule, anaweza asihudhurie tukio hilo, hata hivyo, endapo tukio litatokea nje ya muda ambao mwanafunzi huyo anatumikia adhabu yake ya kufukuzwa nje ya shule, hapaswi kuondolewa kwenye tukio hilo isipokuwa kama kuna wasiwasi wa usalama.